SALA YA JIONI

Wimbo

Cha kutumaini sina, ila damu yake Bwana,
Sina wema wa kutosha, dhambi zangu kuziosha

Kwake Yesu nasimama
Ndiye Mwamba: ni salama x2

Njia yangu iwe ndefu, yeye hunipa wokofu
Mawimbi yakinipiga, nguvu zake ndiyo nanga

Damu yake na sadaka, nategemea daima
Yote chini yakiisha, Mwokozi atanitosha

Nikiitwa hukumuni, Rohoni nina amani
Nikivikwa haki yake, Sina hofu mbele zake
****

(Saburi 121)
Nitainua macho yangu, nitazame milima,
Msaada wangu utatoka wapi?
Msaada wangu u katika Bwana

Bwana ameumba mbingu na nchi
Asiuache mguu wako usongezwe
Hasinzii yeye akulindaye
Haoni usingizi

Bwana ndiye mlinzi wako daima
Yeye uvuli mkono wako wa kuume
Jua halitakupiga mchana
wala mwezi usiku

Bwana atakulinda na mabaya yote
yeye atailinda nafsi yako
Utokapo na uingiapo wewe
Bwana atakulinda
****

Kasisi: Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. (1Yohana 1:8, 9)
****

Kasisi: NDUGU zangu wapemndwa, Maandiko Matakatifu yatuonya mahali pengi, tuzikiri na kuungama dhambi zetu na uovu wetu wa kila namna; tusizifiche wala kuwa na unafiki mbele ya Mwenyezi mungu, Baba yetu wa mbinguni; bali tuziungame kwa moyo mnyenyekevu, uliotubu, na kutii; ili tupate kusamehewa, kwa wema wake na rehema zake zisizo na kikomo. Na ingawa imetupasa kuziungama dhambi zetu mbele ya Mungu kila wakati, lakini zaidi imetupasa kutenda hivi tunapokutana kumshukuru kwa fadhili nyingi tulizopokea kwake, kutangaza sifa zake bora, kusikia Neno lake takatifu, na kumwomba yote yanayohitajiwa kwa mwili na roho. Kwa hivyo nakusihini, nyote mliopo, mfuatane nami kwa moyo safi na kwa sauti ya kunyenyekea, tukikaribie kiti cha neema ya mbinguni;
****

Ungamo lisemwe na wote

BABA Mwenyezi na mwenye rehema, tumekosa na kuacha njia zako kama kondoo waliopotea. Tumefuata mno mawazo na tamaa zetu wenyewe. Tumezihalifu sheria zako takatifu. Tumeyaacha yaliyotupasa kuyatenda. Tumeyatenda yasiyotupasa kuyatenda; wala uzima hatunao. Uturehemu, Wewe Bwana, sisi maskini wenye dhambi. Uwaachilie, Ee Mungu, wanaoungama dhambi zao. Uwarudishe wanaotubu; kwa ahadi zako ulizowaahidia wanadamu katika Kristo Yesu Bwana wetu. Na kwa ajili yake, Ee Baba wa rehema, utujalie tangu leo tuishi maisha ya utakatifu, na ya haki na ya kiasi, kwa utukufu wa jina lako takatifu. *Amin*.
****

***Kasisi*:** MWENYEZI Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, asiyependa mwenye dhambi afe, ila auache uovu wake, awe na uzima; naye amewapa Wahudumu wake mamlaka na amri, wanene kwa uwezo, kwa watu wake wanaotubu, ghofira na ondoleo la dhambi zao; Yeye huwasamehe na kuwaghofiri wote watubuo kwa kweli na kuiamini Injili yake takatifu. Basi, tumwombe, atupe toba la kweli, na Roho wake Mtakatifu, ili mambo tunayotenda sasa yampendeze; na maisha yetu ya tangu sasa yawe safi na matakatifu; na mwisho tufikie furaha yake ya milele; kwa yesu Kristo, Bwana wetu. *Amin*.
****

Anaweza, anaweza Bwana x4
Ameshinda , ameshinda Bwana x4
Ni Mwokozi, ni mwokozi Yesu x4
Aokoa, aokoa Yesu x4
****

Wote wasemesala ya Bwana- pamoja

BABA yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. *Amin*.
****

Kasisi: Ee Bwana, ufumbue midomo yetu;
Jibu: **Na vinywa vyetu vitanena sifa zako**
***Kasisi*:** Ee Mungu, utuokoe kwa haraka;
Jibu: **Ee Bwana, utusaidie hima**
Watu wakiwa wamesimama,

Kasisi: Utukufu una Baba, na Mwana: na Roho Mtakatifu
***Jibu*: Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa: na hata milele ni vivyo. Amin.**
Kasisi:Msifuni Bwana
***Jibu:* Jina la Bwana lisifiwe**
****

Saburi isomwe Kwa pamoja na wote
****

Somo La Agano la Kale
****
Sauti ya Mtu x2
Yalia nyikani tengeneza njia ya Bwana x2
Yanyosheni mapito ya Bwana x4

Sauti ya Yesu x2
Yabisha moyoni sikiapo mfungulie x2
Siufanye moyo kuwa mgumu x4
****

Luka 1:46

MOYO wangu wamwadhimisha Bwana: na roho yangu imemfurahia Mungu, mwokozi wangu.
Kwa kuwa ameutazama: unyonge wa mjakazi wake.
Kwa maana, tazama, tokea sasa : vizazi vyote wataniita mbarikiwa.
Kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea makuu: na jina lake ni takatifu.
Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi: kwa hao wanaomcha
Amefanya nguvu kwa mkono wake: amewatawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao.
Amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi: na wanyonge amewakweza.
Wenye njaa amewashiisha mema: na wenye mali amewaondoa mikono mitupu.
Amemsaidia Israeli, mtumishi wake: ili kukumbuka rehema zake: kama alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele.

Kasisi: **Utukufu una Baba, na Mwana: na Roho Mtakatifu;**
Jibu: **Ulivyokuwa mwanzo, ulivyo sasa: hata milele ni vivyo**. Amin.
****

Somo La Agano Jipya

****

Imani Ya Mitume.na- wote

NAMWAMINI Mungu Baba Menyezi, Muumba wa mbingu na nchi:
Na Yesu Kristo, Mwana wake pekee, Bwana wetu, aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, akazaliwa na Bikira Mariamu, akateswa zamani za Pontio Pilato, akasulibiwa, akafa, akazikwa, akashuka kuzimu; siku ya tatu akafufuka, akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi; kutoka huko atakuja, kuwahukumu watu walio hai nao waliokufa.
Namwamimi Roho Mtakatifu; kanisa takatifu katholiko; ushirika wa watakatifu; ondoleo la dhambi; kufufuliwa kwa mwili; na uzima wa milele. ***Amin.***
****
Kasisi: Bwana akae nanyi
Jibu: **Akae na roho yako**
Kasisi: Na tuombe
Kasisi: Bwana, uturehemu
Jibu : **Kristo uturehemu**
Kasisi: Bwana uturehemu.

Wote waseme Sala Ya Bwana

BABAyetu, uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe makosa yetu, kama sisi tunavyowasamehe waliotukosa. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. ***Amin.***

Kisha Kasisi asimame na aseme.

Kasisi: Ee Bwana, utuonyeshe rehema zako;
Jibu : **Utupe wokovu wako**
Kasisi: Ee Bwana, uwabariki watawala wetu;
Jibu : **Utusikie kwa rehema tukuombapo.**
Kasisi: Uwavike haki wahudumu wako;
Jibu : **Uwafurahishe wateule wako**
Kasisi: Uwaokoe watu wako, Ee Bwana
Jibu : **Uubariki urithi wako**
Kasisi: Utupe amani siku zetu, Ee Bwana
Jibu : **Kwani hakuna mwingine wa kutupigania, ila wewe Mungu wetu**
Kasisi: Ee Mungu, utuumbie ndani mioyo safi;
Jibu : **Wala usituondolee Roho wako Mtakatifu.**

Watu wote waseme

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, ukae nasi sote sasa hata milele. ***Amin.***
****

Wimbo
Neema yake Mwokozi, Pendo za Baba Mwema
Umoja wa Mtulizi, Vije kwetu daima!

Na tupendane vivile, Sisi sote na Mungu
Furaha yetu I tele, Ni furaha ya mbingu

Amenitendea

Amenitendea x4
Imanueli amenitendea x2

Amenipa nguvu x4
Ameniokoa ameniokoa x4

Amenifariji x4
Imanueli amenifariji
****
Tutameta tufanane naye
****
Baraka za Mungu kweli ni za ajabu x2
Zaweza kwenda juu,
Zaweza kwenda chini
Zaweza kwend mbele
Zaweza kwenda chini
Upande , upande kwa mataifa yote x4